MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 26-27/01/2017 ROBO YA PILI (OKTOBA – DESEMBA, 2016).

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	Mh. Namkulya S. Namkulya	-Kata ya Mihambwe	-Mwenyekiti
2.	" Makuyeka B. Salum	-Kata ya Chikongola	-M/Mwenyekiti
3.	" Katani A. Katani	-Mbunge- Tandahimba	-Mjumbe
4.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	"
5.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
6.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
7.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
8.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
9.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
10.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
11.	" Mawazo S. Mbombenga	-Kata ya Nanhyanga	"
12.	" Jamali M.Mtima	-Kata ya Namikupa	"
13.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
14.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya Maundo	"
15.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
16.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
17.	" Ramadhani S. Ulaya	-Kata ya Milongodi	"
18.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
19.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
20.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
21.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
22.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
23.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
24.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
25.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
26.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
27.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
28.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
29.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
30.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
31.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
32.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata ya Mkundi	"
33.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
34.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
35.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
36.	" Amina Issa Mpota	-Viti Maalum	"
37.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
38.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
39.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
40.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"
41.	" Rehema C. Liute	-Viti Maalum	"
42.	" Hawa M. Ramandani	-Viti Maalum	"

43.	“	Amina A. Simba	-Viti Maalum “
44.	Ndg	Said A. Msomoka	- Mkurugenzi Mtendaji (W) Katibu

B: **WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA**

1.	Ndg.	Lazro Matoke	- Kaimu Afisa Utumishi (W)
2.	“	Ally Machela	-Mweka Hazina (W)
3.	“	Issa Naumanga	-Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
4.	Eng:	Paul Mlia	-Mhandisi wa Ujenzi (W)
5.	Dr.	Antipas Swai	-Kaimu Mganga Mkuu (W)
6.	Ndg:	Massau A.J	-Afisa Maendeleo ya Jamii
7.	“	Nosyaga Mwailunga	-Kaimu Afisa Ardhi, Maliasili na Mazingira (W)
8.	“	Edes L. Minja	-Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
9.	“	Marry Kaguo	-Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W)
10.	Eng:	Peter Malekia	- Mhandisi wa Maji (W)
11.	Ndg:	Abdilah Mfinanga	-Afisa Mipango (W)
12.	“	Victor Mkusa	-Kaimu Mkaguzi wa ndani wa Hesabu(W)
13.	“	Mzenga T. Mzenga	-Afisa Elimu Msingi(W)
14.	“	Protas Muhanuzi	-Afisa Manunuzi(W)
15.	“	Bibiana Molenga	-Mratibu wa TASAF
16.	“	James C. Chitumbi	-TEO Tandahimba
17.	“	Judicy Mnizava	- Afisa Mipango
18.	“	Rajabu Athuman	- Afisa Utamaduni
19.	“	Kashen Mtambo	- Afisa Mipango
20.	“	Soud Said	- Afisa Ushirika
21.	“	Geofrey Rutakinikwa	- Afisa Utumishi

C: WAALIKWA

1.	Mh.	Sebastian Waryuba	-Mkuu wa Wilaya Tandahimba
2.	Ndg:	Mohamedi A. Fakili	-Katibu Tawala (W)
3.	“	Thomas Mhecha	-Afisa Usalama (W)
4.	“	Juma A. Lusasi	-Afisa Tarafa Mahuta
5.	“	Rehema Hoza	-Afisa Tarafa Litehu
6.	“	Born Minga	-Afisa Tarafa Namikupa
7.	“	Revocatus M. Friminence	-Meneja Misitu (W)
8.	“	Mbaraka Hittu	-Katibu CUF (W)
9.	“	Abdallah Nalinga	-Mwenyekiti CHADEMA (W)
10.	“	Willy Mkapa	-Katibu CHADEMA (W)
11.	“	Abdul Mtula	-Mwenyekiti CCM(W)
12.	“	Mohamedi Manyamba	-Katibu CCM (W)
13.	“	Ally S. Muwanya	-Mwenyekiti wa Mji Mdogo Tandahimba

D: SEKRETARIATI

1. Christian Mazuge
2. Sofia Nanjota
3. Mohamedi Namkuva

MUHT.NA. 21/2015/2016- KUFUNGUA KIKAO

kabla ya kikao kufunguliwa waliimba wimbo wa Taifa na kusoma dua ya kuiombea Halmashauri wakiongozwa na Mwenyekiti. Katibu aliwakaribisha wajumbe na waalikwa wote kikaoni. Alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 7: 15 mchana.

MUHT.NA. 22/2015/2016- KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda kumi na mbili (12) zilizoandaliwa ziliwasilishwa mbele ya wajumbe wa kikao kwa ajili ya kuzipitia.Baada ya kuzipitia wajumbe waliridhia agenda hizo ambazo ni:-

SIKU YA KWANZA YA BARAZA TAREHE 26/01/2017

1. Kufungua kikao cha Baraza la Madiwani
2. Kuthibitisha agenda za kikao cha Baraza la Madiwani
3. Kupitia taarifa mbalimbali za miradi ya maendeleo ya Kata

SIKU YA PILI YA BARAZA TAREHE 27/01/2017

4. Kujibu maswali ya Wahe. Madiwani ya papo kwa papo
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 27-28/10/2016
6. Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
7. Kujibu maswali ya Waheshimiwa Madiwani ya Maandishi
8. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya kipindi cha Robo ya pili (Oktoba - Disemba 2016)
9. Taarifa mbalimbali za kamati za kudumu za Halmashauri ya Wilaya
    a) Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi
    b) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    c) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    d) Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
10. Taarifa ya matengenezo ya magari
11. Tarifa ya TACOBA
12. Taarifa za Kiutumishi
13. Kufunga kikao

MUHT.NA. 23/2015/2016- KUPITIA TAARIFA MBALIMBALI ZA MIRADI YA MAENDELEO YA KATA

Waheshimiwa Madiwani waliwasilisha taarifa za miradi ya maendeleo kutoka katika Kata zao, Wajumbe walizipokea taarifa hizo. Taarifa hizo zimewekwa katika kitabu kimoja katika kumbukumbu za Halmashauri. Kata zilizowaslisha taarifa ni,

1. Kata ya Chikongola
2. Kata ya Luagala
3. Kata ya Maundo
4. Kata ya Tandahimba
5. Kata ya Litehu
6. Kata ya Mkoreha
7. Kata ya Kitama
8. Kata ya Naputa
9. Kata ya Kwanyama
10. Kata ya Mkonjowano

MJADALA

Mjumbe aliuliza swali kwa nini kuna tatizo la akina mama kujifuangulia Nyumbani katika kata ya kitama.DMheshimiwa Diwani wa kitama alisema tatizo linasababishwa na elimu ndogo ya masuala ya uzazi lakini kwa sasa Elimu imetolewa na wananchi wamekiri na kuahidi kujifungulia katika Zahanati.

SUALA LA MADAWATI

Mjumbe aliuliza chanzo cha tatizo la Madawati katika shule ya sekondari Maundo linatokana na nini wakati tatizo hilo limekwisha kutatuliwa. Mwenyekiti alifafanua kuwa idadi ya Wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne ni wachache wakati walioaingia kidato cha kwanza ni wengi.

USHAURI

Halmashauri itafute ufumbuzi wa Madawati kwani tatizo ni la Wilaya mzima shule za Msingi na Sekondari. Mkurugenzi Mtendaji(W) aliahidi kufanya ufuatiliaji kujua Mapungufu na kuyafanyia kazi.

SUALA LA KUCHELEWA KWA MALIPO YA KOROSHO

Wajumbe walieleza kuwa Kata zote zinakabiliwa na tatizo la kuchelewa kwa malipo na Bei ya Mnada kutofautiana na Bei anayolipwa Mkulima.

Mbunge alieleza kuwa fedha zinaingizwa **TANECU** na hali hiyo wanaijua suala la kucheleweshawa kwa malipo

Baraza liliamua Meneja Mkuu wa **TANECU aitwe kwenye kikao** ili atoe ufafanuzi juu ya Malipo ya Korosho siku ya pili tarehe 27 – 01 -2017.

KUAIRISHA BARAZA
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti aahilishe baraza, Makamu Mwenyekiti aliwashuru wajumbe kwa michango yao. Alisisitiza juu ya **TANECU** kuhudhuria siku ya pili kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa Mauzo ya Korosho. Na kisha kuahilisha baraza muda wa saa 08:13 Mchana.

SIKU YA PILI
Katibu alimkaribisha mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti alifungua kikao muda wa saa 11:48.

TAARIFA
Mwenyekiti alitoa taarifa ya kupata ajali Muheshimiwa Ramadhani Ulaya kupelekwa kulazwa Hospitali ya Wilaya.

SUALA LA MALIPO KWA WAKULIMA.

MASWALI KWA TANECU
Mjumbe aliuliza kwa nini wakulima wanachelewa kupata fedha zao Baada ya mauzo ?
Mjumbe aliuliza sababu ya Bei kuuza Korosho kubadilika/ kutofautiana kutoka kata na kata.?

Mjumbe aliuliza sababu ya wakulima kulipwa kwa Bei ya chini wakati waliuza kwa bei ya juu. Pia waliomba kujua vyama vilivyouza kwa Bei ya juu.

MAJIBU
Kaimu Meneja Mkuu wa TANECU alieleza kuwa Hadi tarehe 27/01/2017 fedha zilizotakiwa kwenda kwa wakulima ni bilioni 200.14 fedha zilizopelekwa ni bilioni 175 sawa na 81%.Fedha ambayo haijapelekwa ni bilioni 40 sawa na 19%
Ilielezwa kuwa fedha ambazo zimebaki meneja mkuu alikuwa hajapata hundi

Sababu zilizochelewesha

- Wingi wa vyama vya msingi
- Utaratibu wa kibenki
- Wakulima wengi kupokea fedha mkononi

Chama cha mzalendo (Mambamba) hakijapeleka fedha kwa wakulima kiasi cha billion 1 ambayo ipo kwenye akaunti ya chama

Pia chama cha majengo hakijalipa bilioni 1.075 kwa wakulima

Sababu za wakulima kupata kwa bei tofauti

Afisa Ushilika alieleza kuwa kilicholipwa kwa mkulima ni kile kilichouzwa kwenye mnada katika msimu wa mwaka 2016/2017 wakulima walilipwa kwa bei ya mnada husika na mabango yamekuwa yakitolewa wazi kwa wananchi wote ili waweze kuona gharama za malipo.

SWALI
Baada ya mzabuni kushinda mnada nani anaingiziwa fedha kati ya chama cha msingi au ni TANECU?.
Mwenyekiti alieleza kuwa mkutano wa wadau wa korosho(Bagamoyo) ilieleza kuwa akaunti itakayotumika kupokea fedha za korosho ni ile inayokubaliwa na bodi ya korosho.

JIBU: Meneja wa TANECU alieleza kuwa akaunti inayopokea fedha ni collection akaunti ambayo itatumika kulipia vyama wanachama wa TANECU maombi hayo yalikubaliwa ili kurahisisha malipo kwa wakulima.

SWALI: Mjumbe aliuliza kuwa kama fedha inaingia kwenye akauti ya TANECU kwa nini ushuru wa halmashauli unalipwa na vyama vya msingi.

MAJIBU: Ilijibiwa kuwa anaetakiwa kulipa kisheria ni vyama vya msingi kwa kuwa ndio wenye fedha na TANECU ni mawakala tu.

SWALI: Mjumbe aliuliza uhusiano wa TANECU na vyama vya msingi.

MAJIBU: Ilielezwa kuwaTANECU imeundwa na vyama vya msingi ambao ndio wamiliki wa wa chama kikuu cha Tandahimba Newala Cooperative (TANECU).

USHAURI
Mjumbe alishauri kuleta wakaguzi wa nje kupitia hesabu za mauzo ya korosho msimu wa 2016/2017.
KUTOLIPWA WANANCHI
Ilielezwa kuwa chama cha Msingi Ghana B kimeingiziwa milioni 58 na walikuwa wanadaiwa shilingi milioni 22 na Bank of Africa (BOA bank) na fedha hizo zimezuiwa na Benki.

MASWALI
Mjumbe aliuliza sababu gani imempelekea Mkuu wa Wilaya kuzuia michango ya wananchi.
JIBU: Mkuu wa wilaya alisema yeye hajazuia shughuli za maendeleo katika kijiji ila alielekeza michango iwe ya hiyari kwa kukubali kupitia mkutano wa kijiji na fedha inayochangwa kutoka kwa wananchi ikatiwe risiti ya selikari.
Pia alishauri vijiji kuwa na sheria ndogo itakayo ruhusu michango hiyo.
SWALI
Kwa kuwa kuna upungufu wa watumishi wa Idara ya Afya ni lini Halmashauri itatoa nafasi za watu wenye sifa kujitolea.
JIBU:Mganga Mkuu(W) Alielezwa kuwa kama kuna mtu mwenye sifa apeleke vyeti kwa ofisi ya Mganga Mkuu (W)

SWALI
Mjumbe aliuliza kuwa Halmshauri ina mpango gani wa kuwezesha mamlaka ya mji mdogo wa Tandahimba kuaanza kufanya kazi zake kikamilifu.

Kaimu Afisa Utumishi(W) Alielezwa kuwa kulikuwa na tafsiri potofu iliofuta halmashauri ya vijiji kinachotakiwa ni kutoa elimu kwa wananchi ili serikali za vijiji ziendelee na kazi.

MUHT.NA. 24/2015/2016- KUTHIBITISHA MHTASARI YA KIKAO VYA TAREHE 27-28/10/2016.

Mhtasari ya kikao cha Baraza la madiwani cha tarehe **27-28/10/2016** uliwasilishwa kwa ajili ya kuupitia na kuuthibitisha. Mara baada ya wajumbe kuupitia mhtasari huo, walikubali kuwa taarifa zilizoandikwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

MUHT.NA. 25/2015/2016- TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI (W)

Mkurugenzi Mtendaji (W) aliwasilisha taarifa yake mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa hiyo ilieleza mambo yafuatayo:-

UJIO WA NAIBU WAZIRI WA TAMISEMI.

Ilielezwa kuwa katika robo ya pili Halmashauri ilitembeLewa na Naibu waziri wa TAMISEMI Mh: Suleiman Jafo. Lengo la ziara ilikuwa ni kukagua na kuhamasisha shuguri za maendeleo pamoja na maelekezo kwa watumishi ili waweze kufanya kai kwa kuzingatia maelezkezo ya serikali.

Pia Halmashauri ya iliweza kuandaa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yenye thamani ya shilingi 32,583,370,013.00 na kupitishwa na baraza la madiwani.

TAARIFA YA MAAFA

Katika robo ya pili Halmashauri ilipata maafa yaliyotokana na mvua na upepo mkali katika vijiji vya Malamba, Miule, Mweru Shuleni,Mkola Juu, Mweru Sokoni, Mkuti, Mnyoma na Tukuru.Maafa haya yalisababisha madhara mbalimbali ikiwemo kupoteza uhai wa mtu mmoja.

SEKTA YA ELIMU

Mkurugenzi Mtendaji (W) alitoa Masikitiko katika sekta ya Elimu kwa sababu Halmashauri ya Tandahimba haikufanya vizuri mtihani wa darasa la saba na kidato cha pili 2016 na kueleza kuwa inabidi kufanya kazi kwa ushirikiano na kila mtu kutimiza wajibu wake ili kuweza kuboresha kiwango cha ufaulu katika Halmashauri yetu.

Taarifa ilipokelewa.

MJADALA

Mjumbe alieleza kuwa kila diwani inabidi awajibike kwenye eneo lake na ashilikiane na watendaji walioko katika eneo lake kuhakikiasha usimamizi mzuri wa Elimu.

MUHT.NA.26 /2016/2017 MASWALI YA WAHESHIMIWA MADIWANI YA AANDISHI

Maswali ya maandishi hayakuwasilishwa.

MUHT.NA.27/2016/2017 –TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA PILI (OKTOBA-DISEMBA, 2016)

Afisa Mipango (W) aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya pili 2016/2017 kwa kueleza kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017. Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imeidhinishiwa kupokea na kutumia jumla ya shilingi 8,356,065,970.00/= katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia , Dira ya maendeleo ya taifa ya mwaka 2025 (vision 2015), Sera mbalimbali za kisekta pamoja na malengo ya maendeleo endelevu (SDG's). Hii ni kutokana na dira na dhima ya Halmashauri kwamba***"Ifikapo 2018 halmashauri ya wilaya ya Tandahimba , kwa kutumia rasilimali zilizopo, utaalam na ushirikishaji wa jamii, iwe imetoa huduma bora kujenga uchumi endelevu utakaowezesha maisha bora ya wananchi"***

Fedha hizo zilitarajiwa kuchangiwa na wadau mbalimbali ikiwemo mapato ya ndani ya Halmashauri (Ownsource), ruzuku ya maendeleo toka serikali kuu (LGCDG), mfuko wa barabara (Road Fund), mfuko kabambe wa afya (health Sector Basket Fund), mfuko wa maji (RWSSP), mpango wa maendeleo ya elimu ya sekondari (Word Bank), Mpango wa maendeleo Elimu Msingi (PEDP), EGPAF, Mfuko wa Jimbo, Pamoja na mfuko wa maendeleo ya jamii (TASAF).

Mchanganuo wa fedha hizo kwa wachangiaji hapo juu kwa mwaka 2016/2017 ni kama unavyoonekana kwenye jedwali hili:-

NA	CHANZO/MCHANGIAJI	MAKISIO	FEDHA TOLEWA	FEDHA TUMIKA	FEDHA ZISIZOPOKELEWA	% YA FEDHA POKELEWA
1	OWNSOURCE	3,304,250,000.00	222,684,978.5	230,954,548.5	3,081,565,021.5	6.7
2	LGCDG	818,851,000.00	143,368,000.0	119,048,000.0	675,483,000.0	17.5
3	MFUKO WA MAJI (NRWSSP)	964,000,000.0	690,118,275.0	691,846,257.0	273,881,725.0	71.6
4	ROAD FUND	1,222,290,000.00	483,277,464.7	483,277,464.7	739,012,535.3	39.5
5	BASKET FUND	484,556.000.00	242,278,999.0		242,278,000.0	50.0
6	PEDP	100,000,000.00			100,000,000.00	0.0
7	MFUKO WA JIMBO	46,991,000.00	43,252,000.0	43,094,000.0	3,739,000.0	92.0
8	TASAF	1,459,485,000.00	775,534,866.5	711,196,040.6	683,950,133.5	53.1
9	WORD BANK	578,164,000.00			578,164,000.0	0.0
10	EGPAF	42,038,970.00	84,579,500.0		-42,540,530.0	201.2
	JUMLA	**9,020,625,970.0**	**2,685,093,084.7**	2,546,029,082.8	**6,335,532,885.3**	**29.8**

Hadi kufikia tarehe 31/12/2016, Halmashauri ilikuwa imepokea na kutumia jumla ya shilingi **2,685,093,084.7** katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 29.8 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2016/2017

Aidha kupitia mfuko wa maendeleo ya jamii TASAF Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 775,534,866.5 na kutumia jumla Tshs. 711,196,040.6 kwa ajili ya malipo ya kaya masikini. Hata hivyo Tshs. 1,132,000.00 zimerejeshwa TASAF Makao Makuu kutokana baadhi ya walengwa kukosa sifa za kulipwa fedha hizo kutokana na vifo au kuhama makazi.

Hadi kufikia tarehe 31/12/2016 Halmashauri imepokea shilingi 199,454,491.30 toka mfuko wa barabara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka 2015/2016.
Taarifa ilipokelewa.

MUHT.NA.28/2015/2016- TAARIFA MBALIMBALI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA

I. KAMATI YA FEDHA, MIPANGO NA UONGOZI

Mwenyekiti wa kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati ya fedha ilivyofanya vikao na agenda zilizojadiliwa. Pamoja na taarifa, iliambatanishwa mihtasari ya vikao vya kamati hiyo na taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Desemba , 2016.
Taarifa ilipokelewa.

YALIYOJITOKEZA

Mjumbe aliuliza hatua iliyofikiwa katika kutekeleza agizo la kuunda kamati ya kufanya uchunguzi ya madai ya vyama vya ushirika.Ilielezwa kuwa kamati ndogo bado inaendeea na kazi na ikikamilisha kazi itawasilisha taarifa.

Mjumbe aliuliza ujenzi wa lami utaanza lini,ilielezwa kuwa mkataba umesainiwa tayari na wakati wowote kazi inaanza.

SUALA LA DUKA LA DAWA

Mjumbe aliuliza hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi wa duka la dawa ilieklezwa kuwa tayari Hospitali imejaza fomu zaa kuomba mkopo NHIF na ukarabati unaendelea.

SUALA LA STENDI MPYA

Ilielezwa kuwa mkataba mpya ulioingizwa mzabuni atalipa laki nane kila mwezi na amepewa sh mashariti ni kuboresha huduma za choo katika eneo la stendi.

II. KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI

Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati ya Elimu, Afya na Maji ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo cha tarehe 07/10/2016.

III. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa iliyoeleza jinsi vikao vya kamati hiyo vilivyofanyika. Pamoja na taarifa, iliambatanisha mhtasari ya vikao vya kamati hiyo vya tarehe 11/10/2016.
Taarifa ilipokelewa.

IV. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati ya Kudhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa hiyo mbele ya wajumbe wa kikao.Taarifa ilieleza jinsi kamati hiyo ilivyofanya vikao vyake. Pamoja na taarifa, uliambatanishwa muhtasari wa kikao cha kamati hiyo wa tarehe 06/10/2016.
Taarifa ilipokelewa.

MUHT.NA.29/2015/2016- TAARIFA YA MATUMIZI YA MAGARI

Ilielezwa kuwa ofisi ys Rais TAMISEMI imeaagiza kusimamia ipasavyo matumizi ya magari pamoja na mali zingine za Halmashauri na kuhakikisha kuwa zinatumiwa kwa maslahi ya umma. Safari zote za kikazi za viongozi wa kisiasa na watendaji wakuu na watumishi ziratibiwe kwa mujibu wa kanuni na miongozo iliyopo.kuhusu uendeshaji wa shughuli za Halmashauri na kumbukumbu za safari zote za kikazi ziwekwe kwenye kitabu cha safari (log book) . Kanuni za Halmashauri zisomwe, zitafailiwe na zieleweke kwa viongozi wa kisiasa na watumishi wote wa wa Halmashauri ili zitekelezwe kikamilifu.
Aidha,upangaji wa magari kwa madereva uzingatie weledi wa taaruma ya utumishi na sio upendeleo au kwa maslahi binafsi ya kiongozi husika. Ofisi ya Rais TAMISEMI haitasita kumchulia hatua za kinidhamu na za kisheria kiongozi au mtumishi yeyote atakaebainika kukiuka kanuni za Halmashauri, taratibu za maadili ya viongozi wa umma Na.13 ya mwaka 1995 na sheria ya utumishi wa umma Na.8 ya mwaka 2002.

Taarifa ilipokelewa

MUHT.NA.30/2015/2016- TAARIFA YA KAMATI YA UFUATILIAJI WA BENKI YA TACOBA

Katibu wa kamati ndogo ya Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya kwa baraza la madiwani kwa kuainisha ufafanuzi toka idara mbalimbali walizofanya nazo mahojiano pamoja na maoini na mapendekezo ya kamati kama ifuatavvyo;

MAONI/ MAELEZO YA KAMATI

1. Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba haipati taarifa za mara kwa mara kuhusiana na maendeleo ya TACOBA
2. Makubaliano ya (MOU) kati ya CRDB na TACOBA yanapunguza nguvu au sauti ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba katika uwakiliahi wa wa wajumbe wa bodi. Wawakilishi wote wa bodi ya Wakurugenzi ni lazima waridhiwe na baraza la madaiwani na mabadiliko yanaweza kufanyika pale halmashauri itakapoona inafaa.
3. Kwa sasa TACOBA haina Mtaji
4. TACOBA ina madeni ya kudaiwa na kudai.

MAPENDEKEZO YA KAMATI

1. Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ibaki na wawakilishi wawili katika bodi ya Wakurugenzi na ukomo wa uwakilishi ni pale mtumishi anapohama, kufa au ukomo wa aina yoyote wa madaraka serikalini
2. Wawakilishi wa Halmashauri katika bodi ya TACOBA watatakiwa watatakiwa kutoa taarifa kwa menejimenti kila baada ya kikao.
3. Hlmashauri iangalie uwezekano wa kuongeza Hisa zake.
4. Mkataba wa jingo baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na TACOBA usisainiwe hadi mapendekezo ya kamati yatekelezwe
5. Kuwepo na kikao cha mwaka cha walezi wa TACOBA ambao ni Halmashauri ya Wilaya na CRDB
6. Wwakilishi wa Halmashauri katika bodi ya Wakurugenzi lazima waidhinishwe na Baraza la Waheshimiwa Madiwani

Tarifa ilipokelewa.

UFAFANUZI MENEJA WA MISITU

Meneja misitu alijitambulisha kuwa yeye ndi meneja misitu Wilaya ya Tandahimba kutoka wakala wa misitu Tanzania(TFS)

Meneja lieleza kuwa ili mtu anunue msitu anatakiwa kupeleka kwa Afisa Misitu(W) hati ya kumiliki aridhi/msitu iliyooidhinishwa na serikari ya kijiji.

Vyombo vinavyosafirisha mazao ya misitu lazima view wazi na muda wa kusafirisha ni kuanzia 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni.

MASWALI

1. Mjumbe aliuliza utaratibu unaotumika kutoza kwa msitu unaomilikiwa na mtu binafsi.
2. Mjumbe aliuliza utaratibu wa kusafirisha mazao ya misitu (samani)
3. Mjumbe aliuliza utaratibu wa kuto vibari
4. Mjumbe aliuliza msitu shirikishi nani anawajibika zaidi kuuhudumia.

MAJIBU

Meneja Misitu alieleza kuwa Gharama zinazotozwa zimegawanyika katika makundi matano na afisa misitu hupiga mahesabu ya hutoza kwa mti ulio simama.
Mtu atatoa aslimia 20% ya vitu anavyo vimiliki, na kwa mti uliotunzwa hutozwa shilingi 70,000/=

Vitu vinatengenezwa ambavyo ni vipya hutozwa kulingana na kifaa kilichotengenezwa ila kwa miti iliyokatiwa lesseni hutozwa shilingi 6000/=.

Usimamizi shirikishi wa misitu huhusisha vjiji husika faini zote hupelekwa kijiji husika na faida itakayotokana na misitu kijiji kinanufaika kwa asilimia 40% na 60% hupelekwa serikali kuu.

Mwenyekiti alimuomba Meneja wa Misitu kupunguza kamata kamata isio na tija kwa wananchi ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuri za maendeleo.

MUHT.NA.31/2015/2016- TAARIFA ZA KIUTUMISHI

I. Mapendekezo ya thibitisha watumishi kazini

Kaimu Afisa Utumishi (w) aliwasilisha Taarifa ya kuomba kuthibitisha Watumishi 19 kutoka Idara mbalimbali.

Baada ya Wajumbe kupitia Tarifa wajumbe walilidhia majina ya watumishi wote yaliyowasilishwa kuthibitishwa kazini.

II. Taarifa ya kuwarejesha watumishi wa Halmashauri ya wilaya Tandahimba

Kaimu Afisa Utumishi (w) aliwasilisha mapendekezo ya kuomba watumishi watatu waliosimamishwa kazi warejeshwe kazini wakati mashauri yao yanaendelea mahakamani.

Watumishi hao ni,

1. Robert E. Mwanawima
2. Marco Ngajua
3. Bakari S. Njunju

Wajumbe baada ya kupitia Taarifa walilidhika na Maombi ya watumishi kurudi kazini.

NASAHA ZA MBUNGE

Mbunge alimsihi Meneja wa Misitu(W) kuendelea kutoa elimu kwa jamii na kuahidi kufanya mizunguko na meneja wa misitu ili kufanya kazi ya kutoa elimu namna ya kuvuna mazao ya misitu.

Alisihi serikali kuridhia wananchi kutoa michango ya hiyari ambayo wananchi wanakubali kwa hiari kuchanga kwa ajiri ya kuanzisha miradi ya Maendeleo.

Alisihi viongozi wa serikali kushirikiana na wanasiasa kutekeleza shughuliza kimaendeleo ya wilaya ya Tandahimba.

MAKAMU MWENYEKITI

Alisistiza viongozi wakuu kufanya mawasliano na viongozi wa kata husika na kuomba kuweka kando tofauti za kisiasa katika shughuli za kuleta maendeleo ya wilaya.

Aliomba viongozi wa serikali pamoja na mwenyekiti wa Halmashauri kwenda Chingungwe kushughulikia tatizo la mgogoro ya ardhi uliopo shule ya Secondari Chingungwe.

NASAHA ZA MKUU WA WILAYA

Alishauri wajumbe kuwa na ushilikiano wakati wa kikao na kusema kuwa maendeleo yataletwa na wananchi wenyewe.

Alisisitiza yeye hajazuwia michango kwa wananchi bali aliagiza taratibu kufuatwa kuchangisha hiyo michango na iwe imeridhiwa na wananchi wenyewe na zitolewe stakabadhi za selkari wakati wa kupokea michango.

SUALA LA MAZAO YA MISITU

alieleza kuwa wananchi wasiezuliwa mbao ambazo wamesha ezeka pia Afisa Misitu(W) kuhamasisha wananchi kuwa na vibali vya kuuza mazao ya missitu hususani mbao amabvyo vitawawezesha kuuza mbao kwa bei rahisi inayoendana na mazingira

aliwashauli wajumbe kuendelea kushirikiana na kupinga tamaduni mbovu zinazochochea kushuka kwa elimu.

Alishauli dampo lililopo lichimbwe na lianze kufanya kazi mapema iwezekanavyo

Alishauli suala la TACOBA liangaliwe kwa uzuri na maamuzi yenye tija yaamuliwe kwenye vikao halali vya TACOBA.

Suala la mgogoro wa ardhi Chingungwe aliagiza afisa ardhi kufatilia suala la mgogoro na kutoa taarifa kwa mkuu wa ailaya.

HALI YA CHAKULA

Ilielezwa kuwa kataika msimu wa 2016/2017 wananchi wa Tandahimba wamevuna korosho za kutosha na kuuza kwa bei nzuri hivyo kufanya kuwa na uchumi imara na pia wanajihusisha na ulimaji wa zai la Mhogo na kwa hali ilivyo Tandahimba haina njaa.

MUHT.NA.32/2015/2016- KUFUNGA

Mwenyekiti alisisitiza mkurugenzi kutekeleza mambo yaliyo amuliwa kwenye kikao na kufunga kikao muda wa saa 9:45 mchana.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA

JINA

MWENYEKITI

SAINI

JINA

KATIBU

SAINI

28-04-2017

TAREHE